

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUVUMA
Simu Nambari. 025-2602256/2602238
Fax No. 2602144



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L. P. 74,
SONGEA.

TAARIFA KWA UMMA

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Christina Mndeme anapenda kuutarifu umma na wadau wote wa maendeleo kuwa **Maonyesho ya Viwanda na Uwekezaji yaliokuwa yafanyike tarehe 03 hadi 09 Desemba 2018** katika uwanja wa Zimanimoto Manispaa ya Songea yamesogezwa mbele.

Mheshimiwa Mndeme ametaja sababu ya kuahirisha ni kutokana na taarifa za hali ya hewa kuonyesha kuwa katika kipindi cha mwezi Desemba 2018 Mkoa wa Ruvuma unategemea kuwa na mvua nyingi. Tarehe mpya ya maonyesho imepangwa kuwa **Mwezi Mei, 2019**.

Wadau wa uwekezaji, wenye Viwanda, Wajasiliamali, Taasisi za Umma na binafsi wote mnaombwa kuendelea kujiandikisha na kuwasilisha uthibitisho wenu wa kushiriki kwenye maonyesho yajayo.

Kauli mbiu ya maonyesho haya ni **“Ruvuma Itavuma kwa Uchumi wa Viwanda, Wekeza Sasa”**

Imetolewa na ;

Revocatus A. Kassimba
Afisa Habari

**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Ruvuma
Songea**

27 Novemba, 2018